# Usalama Pamoja

Sera ya ICYE inayo shughulikia ukatili wa kijinsia katika kazi za kujitolea za kimataifa

International Cultural Youth Exchange

ICYE

# Yaliyomo


**Utangulizi** **1**

Mwathirika dhidi ya Manusura 2

Madhumuni 3

Upeo 3

Kanuni za Jumla 4

**Kuzuia Ukatili wa Kijinsia** **6**

Sababu za Hatari 6

Mikakati ya Ukingaji 7

**Kushughulikia Ukatili wa Kijinsia** **9**

Utaratibu wa Malalamiko 9

Kuwasaidia Manusura 10

Vikwazo na Hatua za Nidhamu 12

**Wajibu wa ICYE** **14**

Wajibu wa Utunzaji 14

Wajibu wa vikundi mahusus vya wadau 15

**Utekelezaji wa Sera hii** **22**

Msaada wa kifedha 22

Ufuatiliaji na Tathmini 23

**Mafafanuzi** **24**

# Utangulizi[1]

ICYE imejidhatiti kutoa mazingira salama kwa kila mtu ambaye anafanya kazi au kushirikiana na ICYE ambayo haina ubaguzi na ukatili. Sera hii inashughulikia suala la ukatili wa kijinsia, ikiwemo unyanyasaji wa kingono.

Sera inasisitiza kwamba ICYE itatumia sera ambayo haifumbii macho aina yoyote ya ukatili wa kijinsia. Hatua za kuzuia na kushughulikia unyanyasaji zilizoelezwa katika sera hii zina lengo la kutoa ulinzi kwa ajili ya aina zote za ukatili wa kijinsiakwa kila mtu anayeshirikiana na ICYE.

ICYE inakiri kwamba mtu yeyote anaweza kuwa mwathirika wa ukatili wa kijinsia, bila kujali jinsia yake wala jinsia ya mhalifu wake. Tunatambua kwamba unyanyasaji wa kijinsia ni dhihirisho la nguvu ya mahusiano na mara nyingi hutokea katika muktadha wa mahusiano, ikimaanisha kwamba mara nyingi waathirika na wahalifu huwa wanafahamiana. Kazini au wakati wa kujitolea mara nyingi hutokea katika mahusiano yasiyo sawa, kwa mfano kati ya meneja na msimamizi, wafanyakazi na wafanyakazi wa kujitolea.

Mbali na makosa ya jinai yanayofahamika kisheria hakuna mashauri "ya kweli" kuhusu aina ya tabia au hali ambayo inaonekana kama ukatili wa kijinsiana mtu fulani, zaidi ya hayo sababu ya uamuzi ni hukumu binafsi ya mtu aliyeathiriwa.

ICYE inaahidi kumtendea kwa heshima kila mtu anayewasilisha malalamiko, kuyaamini na kuyashughulikia kwa uzito unaofaa malalamiko hayo. Madai yote yatachunguzwa haraka kwa mujibu wa manusura na sheria.

1 Rasimu hii imejikita kwenye kazi za kimataifa na kazi nzuri za ICYE. Ikiwemo sera zilizopo za ukatili wa kijinsia kutoka Care, Oxfam na Plan International, kipeperushi cha habari kwa wafanyakazi wa kujitolea kutoka Weltwärts pamoja na matokeo ya warsha kuhusu unyanyasaji wa kijinsia iliyofanywa na ICJA na washirika, iliyofanyika Berlin, Ujerumani Oktoba 2018.

Hakuna hatua itakayochukuliwa bila idhini ya manusura - isipokuwa kama ni lazima kisheria kuripoti (kwa mfano ikiwa manusura ni watoto). Wafanyakazi wa ICYE au wafanyakazi wenza watakaobainika kwamba wamemfanyia ukatili au wamemnyanyasa kingono mtu mwingine watachukuliwa hatua za kiutawala au za kinidhamu, hadi na ikiwemo kufukuzwa kazi vilevile kupelekwa kwenye mamlaka husika kwa ajili ya kuchukuliwa hatua zaidi, ikiwemo kufunguliwa mashtaka ya jinai. Pia, mtu mwingine yeyote anayeshirikiana na ICYE atapata madhara (kwa mfano kusitisha ushirikiano) vilevile kupelekwa kwenye mamlaka husika ili kuchukuliwa hatua zaidi, ikiwemo kufunguliwa mashtaka ya jinai.

Sera ya ICYE inayopinga ukatili wa kijinsia ya " Usalama Pamoja " inalenga kumlinda kila mtu anayeshirikiana na ICYE dhidi ya aina yoyote ya ukatili wa kijinsia.

Hakuna aina yoyote ya ukatili wa kijinsia, ikiwemo unyanyasaji wa kijinsia, itakayovumiliwa hapa ICYE. Utamaduni wetu wa kazi unategemea kuheshimiana na ushirikiano na tunakataa aina zote za ukatili wa kijinsiaa kama ukiukaji mkubwa wa haki, utu na thamani ya kila mtu.

Sera hii itajumuisha fasili na mifano ya ukatili wa kijinsia, maelezo kuhusu taratibu za malalamiko na jinsi ya kuripoti matukio hayo, muhtasari wa uchunguzi na michakato ya kinidhamu na haki za watu wanaoshirikiana na kazi yetu. Pia inaeleza wajibu wetu, jinsi tunavyoshughulikia madai, tunavyozuia ukatili wa kijinsia na kuwasaidia manusura kurejea katika hali zao za kawaida.

# Mwathirika dhidi ya Manusura

Katika sera hii, tunatumia maneno 'mwathirika' na 'manusura', kwa kuwa tunakiri kwamba yanatimiza malengo tofauti.[2] Neno 'mwathirika' mara nyingi hutumika katika miktadha ya kisheria, ambapo mtu amefanyiwa uhalifu ambao umetekelezwa na mhalifu. Watu ambao wamepata ahueni dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijin-

2 Kulingana na https://sakitta.org/toolkit/docs/Victim-or-Survivor-Terminology-from-Investigation-Through-Prosecution.pdf and https://www.unwomen.org/en/what-we-do/ending-violence-against-women/faqs/types-of-violence

siaingawa kimsingi huenda hawataki kutafsiriwa kama mtu ambaye amefanyiwa uhalifu lakini badala yake anaonyesha uthabiti na kumiliki mchakato wake wa uponyaji. Ndiyo maana watu wengi wanapendelea neno 'manusura'.

ICYE inakiri kwamba ni jukumu la mtu aliyekabiliwa na ukatili wa kijinsia kufasiri neno hilo na tutaheshimu maneno yake.

> *""Manusura ni neno ambalo huniwezesha na kuniruhusu kuelezea kwamba nimepitia majaribu, lakini hatimaye nimenusurika. Hakika mimi huwa natumia neno mwathirika, hasa ninapoelezea kuhusu shambulio lenyewe. Ninatumia neno mwathirika kueleza kwamba uhalifu huu ni wa kutisha, unabadilisha maisha, unamwathiri kila mtu aliye karibu na ninayempenda.*
> *Nafikiri kile ambacho kimekuwa muhimu sana katika safari yangu yote, bila kujali yule ninayezungumza naye—iwe ni wakili, mpelelezi, au mwendesha mashtaka na neno lolote wanalotumia wanapozungumza nami. Hicho sio ninachokumbuka—ninachokumbuka ni wema, kujali, subira; hilo ndilo jambo muhimu zaidi.""*
>
> **Manusura wa Shambulio la Ngono[3]**

# Madhumuni

ICYE imejidhatiti hasa kukuza utamaduni na mazingira ya shirika salama na mazuri kwa watu wote na mbinu isiyovumilia ukatili wa kijinsia, ikiwemo ukatili wa kijinsia. Lengo ni kuwalinda wafanyakazi, wafanyakazi wenza, wafanyakazi wa kujitolea, washirika, wanajumuiya na wadau wengine wanaoshirikiana na ICYE dhidi ya tabia isiyotakiwa ya unyanyasaji wa kingono na ukatili wa kijinsia wa aina zote.

3 https://sakitta.org/toolkit/docs/Victim-or-Survivor-Terminology-from-Investigation-Through-Prosecution.pdf

# Upeo

Sera hii inatumika kwa wafanyakazi wote wa ICYE, wafanyakazi wenza na wajumbe wa bodi pamoja na kila mtu anayewasiliana na ICYE, ikiwemo wafanyakazi wa kujitolea, wanafunzi wa mafunzo kazini, washirika, wanajumuiya, wageni, washauri, makandarasi, watoto na vijana - bila kujali jinsia zao, mwelekeo wa kijinsia, elimu, darasa, kazi, ukuu na hadhi. ukatili wa kijinsia hautavumiliwa

ndani au nje ya eneo la ICYE. Sera hii itatumika muda wa kawaida wa kazi pamoja na nje ya muda wa kawaida wa kazi.

ICYE imejitolea kutekeleza vipengele vyote vya sera hii na kufuatilia ufanisi wake. Pia tutashirikisha miradi ya mwenyeji. Tutashirikiana na mashirika ya wataalam

# Kanuni za Jumla

**Hakuna mwenye haki ya kumnyanyasa kingono au kukiuka mtu yeyote.** Aina yoyote ya ukatili wa kijinsia ambayo ICYE itaibaini, itashughulikiwa kwa heshima na uwazi kwa mwathirika. Mtu yeyote ndani ya ICYE, ambaye atapatikana na hatia ya kufanya unyanyasaji wa kijinsia, atachukuliwa hatua za kinidhamu, hadi na ikiwemo kufukuzwa kazi vilevile kufunguliwa kesi ya jinai.

**ICYE inaamini kwamba ukatili wa kijinsia sio mdogo hata kuushughulikiwa.** Aina yoyote ya ukatiri au ukatili wa kijinsia unaweza kuwadhoofisha wafanyakazi wa kujitolea, wafanyakazi, wafanyakazi wenza, washirika na wanajumuiya na kutengeneza mazingira ya uadui. Kila madai yatasikilizwa na waathirika wataaminiwa na kusaidiwa.

**ICYE itafanya kila kitu kuzuia ukatili wa kijinsia na kuwalinda manusura dhidi ya unyanyasaji au lawama zaidi.** Ikiwa wafanyakazi, wafanyakazi wenza au wafanyakazi wa kujitolea wataripoti kuhusu ukatili wa kijinsia waliopitia, ICYE inatoa hakikisho la kushughulikia suala hilo kwa siri. Watasaidiwa kikamilifu na hakutakuwa na hatua mbaya dhidi yao.

**ICYE itahakikisha kwamba kila malalamiko yatafuatiliwa.**
Wafanyakazi wa ICYE, hasa wakurugenzi na mameneja wa ofisi, wanalazimika kuchukua hatua wanapokuwa na mashaka au wanapopokea ripoti. Kuiacha tabia hii iendelee au kuihamasisha, itasababisha uchukuliwe hatua za kinidhamu. Mfanyakazi yeyote au wafanyakazi wenza wowote wa ICYE ambaye anashuhudia tukio la ukatili wa kijinsia, ikiwemo ukatili wa kijinsia, au ana uthibitisho wa aina nyingine, lazima aripoti hili kwa mujibu wa utaratibu wa malalamiko ulioelezwa hapa chini. ICYE itazisaidia mamlaka za kitaifa kuhusiana na uhalifu wowote uliofanyika.

**ICYE itaheshimu ridhaa na matakwa ya manusura katika hatua yoyote inaposhughulikia madai hayo.**
Kwa kuwa ukatili wa kijinsia humuathiri mtu, ni muhimu sana kuheshimu na kurejesha uhuru wa mtu. Kwa hivyo, ICYE itahakikisha kwamba manusura anashirikishwa na kufahamishwa kadri wanavyotaka. Wafanyakazi wa ICYE watahakikisha kwamba watu wote wanaohusika wanafahamu kuwa matukio yote ya ukatili wa kijinsia yanaripotiwa kwa siri kila mwaka kwenye Serikali Kuu.
Kwa ICYE mwathirika anaweza kuamua ni kiasi gani anataka kushirikishwa katika mchakato mzima na kwa hakika hatutachukua hatua bila idhini yake. Pia bado tunatambua kwamba kunaweza kuwa na matukio ambapo ni muhimu au lazima kuchukua hatua za kisheria, kwa mfano pale ambapo watoto wanahusika au inapohitajika kulinda usalama wa mtu. Kila NC inapaswa kuamua kwa misingi ya mtu mmoja-mmoja jinsi ya kushughulikia kila jambo mahususi na atafanya hivyo kwa kushirikiana kwa karibu na mashirika/mamlaka iliyobobea ili kumsaidia manusura na ICYE katika mchakato wa kufanya maamuzi.

# Kuzuia Unyanyasaji Kijinsia[4]

Athari za ukatili wa kijinsia kwa mtu mara nyingi huwa mbaya sana na zinaweza kuwa na athari za kudumu kwa mwathirika pamoja na mazingira yake.[5] Sera ya ICYE isiyovumilia aina yoyote ya ukatili wa kijinsia hivyo inaanza na kinga ya msingi ambayo ndiyo msingi wa dhamira yetu ya kutoa mazingira salama kwa kila mtu anayefanya kazi au kushirikiana na ICYE.

> Kinga ya msingi inapinga mitazamo na kanuni zilizopitwa na wakati na za kuwalaumu waathirika ambazo kwa mfano kuweka mkazo kwa waathirika wanaoweza kutokea kujilinda na kuuangalia ukatili wa kijinsia kama tatizo la afya ya umma pekee. Mikakati madhubuti ya kuzuia unyanyasaji inalenga kubadilisha mitazamo ya ndani ya kibaguzi, mifumo ya tabia ya ukatili na mifu¬mo ya kitamaduni, kisiasa, kiuchumi na kijamii inayowezesha unyanyasaji wa kijinsia.

Sera hii peke yake haitazuia kabisa matukio ya ukatili wa kijinsia kutokea, lakini ni msingi wa miongozo yetu ya utekelezaji katika kuzuia na kushughulikia matukio kama hayo. Jitihada endelevu za kuzuia unyanyasaji, kwa kiwango kikubwa zitajenga mazingira ambayo ukatili wa kijinsia unatambulika kama jambo lisilokubalika na manusura watakuwa tayari zaidi kuripoti kuhusu waliyopitia.

4 Pia tazama: https://www.cdc.gov/violenceprevention/pdf/SV-Prevention-Technical-Package.pdf

5 GIZ inakadiria kwamba unyanyasaji dhidi ya wanawake nchini Peru, kwa mfano huzalisha na hasara ya mwaka ya zaidi ya dola za Marekani bilioni 6.7 kutokana na kupotea kwa siku za kazi milioni 70 ambazo ni sawa na upotevu wa 3.7/ ya Pato la Taifa https://www.giz.de/en/worldwide/12205.html

# Mambo ya Hatari

Ni muhimu kuelewa na kuchambua visababishi ambavyo huongeza hatari ya uwezekano wa kuwa mwathirika au mhalifu wa ukatili wa kijinsia.[6] Kwa kawaida mambo haya huchochewa na sababu mbalimbali zinazohusiana katika ngazi ya mtu binafsi, jamii na mfumo.

Katika ngazi ya taifa, ni wajibu wa kila Kamati ya Kitaifa (NC) angalau kufahamu mambo ya hatari katika eneo lao linapokuja suala la ukatili wa kijinsia. Maarifa haya hayataelezea tu michakato yao ya kulinganisha na upangaji, lakini pia itawawezesha kuandaa na kutunga hatua za tahadhari, kama vile mafunzo au ujumbe lengwa ambao ni wa kipekee katika eneo lao la kazi. Katika baadhi ya jamii, kwa mfano wanawake weupe wanaonekana kama wazi¬nzi - jambo ambalo linaweza kuwaweka wanawake weupe wanaojitolea katika hatari huku kwa wengine, wanawake weusi wanachukuliwa kuwa wafanyabiashara ya ngono, pia wapo katika hatari ya kufanyiwa ukatili wa kijinsia.

# Mikakati ya Kuzuia

Hatua za kuzuia ndani ya Shirikisho huanza moja kwa moja kuanzia kwenye mchakato wa kuwaajiri wafanyakazi wa ICYE, wafanyakazi wenza na wafanyakazi wa kujitolea na huendelea katika kipindi chote cha programu yetu.

Sehemu muhimu ya kazi yetu ya kuzuia ni kuongeza ufahamu na mafunzo. ICYE inajitolea kuwa na nia ya kutuma ujumbe mtandaoni na nje ya mtandao. Jinsi tunavyolishughulikia suala hili katika mafunzo ya ICYE au kanuni za kawaida za maadili kwa mfano, kutasisitiza ujumbe wetu wa pamoja wa kutovumilia unyanyasaji wa kijinsia. Elezea tokea mwanzo kwamba ukatili wa kijinsia unatazamwa kwa uzito na hushughulikiwa kwa njia inayofaa ambayo husaidia kuunda utamaduni wa shirika ambapo manusura wako radhi kuzungumza kuzungumza kuhusu yale waliyopitia, kwa kuwa kutakuwa na uwezekano mkubwa kwao kuamini kwamba shirika

6 Tazama mifano ya mambo ya hatari hapa: https://www.nsvrc.org/sites/default/files/publications/2019-04/Risk%20%26%20Protective%20factors.pdf

litashughulikia ipasavyo matukio hayo. ICYE inaahidi kwenda mbali zaidi katika kujenga uelewa kuhusu uzito wa suala hilo hasa katika. jamii ambayo mada ya ukatili wa kijinsia inaelekea kupuuzwa au kutotiliwa maanani.

ICYE itahakikisha kwamba sera hii inasambazwa kwa wingi kwa watu wote wanaohusika. Warsha za kimataifa za mafunzo ya wakufunzi zitaandaliwa na Ofisi ya Kimataifa ambapo washiriki watapewa zana na ujuzi wa jinsi ya kushughulikia ripoti za ukatili wa kijinsia ipasavyo. Sera hii itajumuishwa katika Mwongozo wa NCs na, kama itakuwepo, katika kila kitabu cha mwongozo cha wafanyikazi wa NC. Kila NC itawapa mafunzo wafanyakazi wake na wafanyakazi wenza wote kuhusu maudhui ya sera hii na kuhakikisha kwamba wafanyakazi wote wanaojitolea na waandaji wanafahamu maudhui ya sera hii. Vipindi vya kukuza ufahamu vitajumuishwa katika mipango ya utangulizi na mawasiliano ya kawaida ya ndani.

Kila baada ya miaka miwili, ICYE itahitaji wafanyakazi kuhudhuria mafunzo ya mtandaoni ya kujikumbushia kutoka Ofisi ya Kimataifa kuhusu maudhui ya sera hii.

# Kushughulikia Ukatili wa Kijinsia

## Utaratibu wa Malalamiko

### Tunasikiliza!

Ukatili wa kijinsia unaweza kuwachosha wale wanaouvumilia. Kuzungumzia suala hili mara nyingi ni jambo gumu kwa kuhofia kutosikilizwa, kuwakasirisha mameneja na kupinga utamaduni wa shirika. Tafadhali usiruhusu hofu hizi zikuzuie. ukatili wa kijinsia wa kijinsia, huku pia ikikulinda dhidi ya ulipizaji kisasi pindi unaporipoti matukio ya ukatili wa kijinsia kwa nia njema. NC wa ICYE wanapaswa kujua kinachoendelea ili waweze kukifanyia kazi. Kupaza sauti yako kunaweza kunaweza kuwa hatua muhimu ya kukabiliana na mambo ambayo umeyapitia, kunaweza kuwa sehemu ya uwezeshaji wako mwenyewe na kunaweza kuchangia kuzuia watu wengine kufanyiwa unyanyasaji.

ICYE itahakikisha kwamba madai yote ya ukatili wa kijinsia, ikiwemo ukatili wa kijinsia, yanachunguzwa kwa kina na ikihitajika, kuchunguzwa na/au kupelekwa kwenye shirika jingine kwa ajili ya uchunguzi au kuripotiwa kwenye vyombo vya sheria.

Masuala hayo yanaweza kuripotiwa katika moja ya njia zifuatazo:

- Mtu anayetaka kuripoti suala la ukatili wa kijinsia ndani ya maeneo yao au familia mwenyeji, anaweza kutoa taarifa moja kwa moja NC Mwenyeji au kupitia mtu wanayemwamini. Iwapo tukio litatokea ndani ya NC mwenyeji, NC inayotuma inapaswa kuarifiwa.

- Masuala hayo yanaweza kuwasilishwa kwa ofisa wa ICYE aliyeteuliwa rasmi na kupatiwa mafunzo au kwa mtu fulani ndani ya ICYE ambaye mlalamikaji anamwamini. Mara nyingi jambo hili husaidia kuamua hatua inayopaswa kuchukuliwa.
- Masuala hayo pia yanaweza kutumwa moja kwa moja kwenye Ofisi ya Kimataifa ya ICYE ambayo itashughulikia masuala yote kwa usiri unaohitajika na kulingana na ahadi zilizo katika sera hii: reporting-cases@icye.org
- Pia, unaweza kutumia njia za malalamiko za mahali ulipo au za kitaifa au mashirika yaliyobobea (kama vile mashirika ya haki za wanawake) au kwa kuwasiliana na:
  - Mtu yeyote unayemwamini na ambaye anaweza kuwasiliana na mwakilishi wa ICYE
  - Mchunguzi Maalum[7]
  - Mahakama ya Kazi
  - Kamati yako inayotuma
  - NGO ya kitaifa au ya kimataifa inayoshughulikia mada hii

Maafisa walioteuliwa wa ICYE wanapofahamishwa kuhusu tukio linalohusisha ukatili wa kijinsia:

- kulingana na kile mwathirika anachokihisi, watahakikisha kwamba wako salama na kutoa msaada wa kihisia,
- watafafanua hitaji la uchunguzi wa kitabibu (kwa mfano, kwa sababu ya magonjwa ya kuambukiza, ushahidi wa manii, itifaki ya majeraha, kuzuia ujauzito)
- watafafanua hitaji la msaada na matibabu ya kisaikolojia ya kitaalamu ya nje,
- watafafanua hitaji la msaada wa kisheria,
- kulinda usiri ilimradi tu hakuna tishio la afya au usalama kwa watu hao au mtu mwingine yeyote,

7 Mchunguzi Maalum ni mtu ambaye anachunguza, anaripoti na kusaidia kutatua malalamiko.

- kuthibitisha maoni ya mwathirika kuhusu hatua wanayotaka kuchukua na mtu anayepaswa kujulishwa/kushirikishwa katika mchakato huo,
- kuhakikisha kwamba mwathirika anaelewa taratibu za shirika za kushughulikia malalamiko,
- kuandika tarehe, nyakati na ukweli wa tukio/matukio, ilimradi tu ni muhimu na inawezekana kwa mwathirika,
- kujadili na kukubaliana na hatua zinazofuata: iwe malalamiko yasiyo rasmi au rasmi - kwa kuelewa kwamba kuchagua kutatua suala hilo kwa njia isiyo rasmi hakumzuii mwathirika kufuata njia rasmi ya kutatua malalamiko ikiwa hajaridhika na matokeo,
- kuhifadhi taarifa ya siri katika mijadala yote ilimradi tu inahitajika katika uendeshaji wa kesi na ilimradi tu mtu anayehusika hapingi,
- wataheshimu chaguo la mwathirika katika kila hatua na usijaribu kubishana au kuwashawishi au kuwashawishi wakati wowote,
- watahakikisha kwamba wanajua kuwa wanaweza kuwasilisha malalamiko nje ya shirika kupitia nchi/mfumo husika wa kisheria,
- ikiwa ni kuhusu mfanyakazi wa kujitolea wa kimataifa, wajulishe NC husika na tuma nakala kwenye IO.

# Vikwazo na Hatua za Nidhamu

Madhumuni ya sera hii ni kuwalinda waathirika wote huku pia ikiendeleza mbinu ya kitaalamu katika ufuatiliaji wa kila kesi inayoweza kutokea:

Iwapo **wafanyakazi au wafanyakazi wenza wa ICYE** wanashutumiwa kutenda kitendo chochote cha ukatili wa kijinsia kwa mtu yeyote na kama ilivyoelezwa katika sera hii, NC husika inapaswa kumsimamisha kazi mfanyakazi au mfanyakazi mwenza ili kupisha uchunguzi. Iwapo hatua hii haitafuatwa, NC itapaswa kuhalalisha uamuzi wake kwa maandishi kwa BoM na IO. Endapo madai hayo yatathibitishwa, NC itachukua hatua za kinidhamu ili kuhakikisha uthabiti wa matukio yote ya ukatili wa kijinsia kulingana na sera hii na kwa mujibu wa sheria za nchi.

Iwapo **mwakilishi au mfanyakazi wa mradi mwenyeji au mwanafamilia mwenyeji** anatuhumiwa kwa kitendo chochote cha ukatili wa kijinsia kwa mtu yeyote na kama ilivyofafanuliwa katika sera hii, NC inapaswa kusitisha mara moja ushirikiano na mradi mwenyeji au familia mwenyeji ili kupisha uchunguzi. Iwapo hatua hii haifuatwi, na NC ikaamua kuendeleza ushirikiano na mradi au familia mwenyeji, itapaswa kuthibitisha uamuzi wake kwa maandishi kwa BoM, IO na NC yoyote husika. Iwapo madai yamethibitishwa na ni sahihi kwa mujibu wa sheria ya jinai ya nchi, NC itamsaidia mwathirika iwapo anataka kuchukua hatua za kisheria na pia kushirikiana na mamlaka ya nchi, ikihitajika.

Iwapo **mfanyakazi wa kujitolea** anatuhumiwa kufanya kitendo chochote cha ukatili wa kijinsia kwa mtu yeyote na kama ilivyoelezwa katika sera hii, NC inapaswa kuwaondoa kwenye mradi wa mwenyeji na familia mwenyeji ili kupisha uchunguzi. Iwapo hatua hii haijafuatwa na mfanyakazi anayejitolea kuruhusiwa kuendelea na mradi, basi NC mwenyeji itapaswa kuthibitisha uamuzi wake na kuijulisha NC inayotuma na IO. Iwapo madai yamethibitishwa, wafanyakazi wa kujitolea wanaweza kuchukuliwa hatua za kisheria au hatua nyingine zilizobainishwa katika nchi mwenyeji.

Hatua nyingine za mabadiliko kama vile shughuli za elimu au haki ya urejeshaji itachunguzwa kwa misingi ya jambo husika.

## Kuwasaidia Manusura

Mbali na kusaidia kuzuia na kukabiliana na matukio hayo, msaada utatolewa kwa manusura wa ukatili wa kijinsia. Hii inaweza kujumuisha kupelekwa kwenye mashirika ya wataalam, matibabu, msaada wa kisheria, likizo ya ugonjwa, msaada wa kisaikolojia na kijamii au fidia ya kifedha kwa mujibu wa sheria. Mbinu inayomlenga manusura[8] itakuwa muhimu katika mbinu yetu.

ICYE itahakikisha kwamba nafasi na haki za manusura hazitahatarishwa wala kubadilishwa iwapo njia yoyote kati ya zilizo hapo juu au njia nyingine za msaada zitatumika.

8 "Mbinu inayowalenga manusura inakusudia kutanguliza haki za kila manusura katika hatua zote na kuhakikisha kwamba kila manusura anaheshimika na kujali utu wake. Kwa kumpa kipaumbele manusura katika mchakato huu, mbinu hiyo inachochea arudi katika hali yake ya kawaida, hupunguza hatari ya kutokea madhara mengi zaidi na huimarisha shirika lake na kujitawala. Kutumia mbinu inayomlenga manusura kunamaanisha kuanzisha uhusiano na manusura ambayo huimarisha usalama wao wa kihisia na kimwili, hujenga uaminifu na huwasaidia kurejesha udhibiti fulani wa maisha yao. https://www.unicef.org/eca/media/15831/file/Module%202.pdf

# Wajibu wa ICYE

## Wajibu wa Uangalizi

> Hapa ICYE tunafahamu wajibu wetu kuhusu kuzuia na kukabiliana na ukatili wa kijinsia. Tunatofautisha kati ya "wajibu wa kisheria wa uangalizi" na "wajibu wa kimaadili wa uangalizi". "Wajibu wa kisheria wa uangalizi" unamaanisha vitendo ambavyo watu au mashi¬rika yanalazimika kuvifanya kama ilivyobainishwa na sheria. "Wajibu wa kimaadili wa uangalizi" unamaanisha vitendo ambavyo watu au mashi¬rika yanapaswa kuvifanya kwa sababu ni jambo sahihi kulifanya.

Kwa kuzingatia hali ya mahusiano ya kazi kati ya wafanyakazi, wafanyakazi wa kujitolea, wafanyakazi wenza, familia mwenyeji, miradi na jumuiya mwenyeji wa ICYE mara nyingi kutakuwa na jukumu la pamoja la kisheria na la kimaadili la uangalizi wakati wowote tukio linapotokea. Pia tunakiri kwamba ikiwa mwanajamii ambaye hana uhusiano wa moja kwa moja na ICYE ataripoti suala la ukatili wa kijinsia kwetu, bado tuna wajibu wa kumhudumia mtu huyo.

Kwa ujumla, kila mtu anayefanya kazi au anayeshirikiana na ICYE (kwa mfano wajumbe wa bodi, wafanyakazi na wafanyakazi wenza, wafanyakazi wa kujitolea, miradi na familia wenyeji) anapaswa kusaini kwamba amepewa taarifa kuhusu Sera ya ICYE ya " Usalama Pamoja " na kwamba anaahidi kuisimamia. Inatarajiwa kwamba hakuna mfanyakazi wa ICYE wala mfanyakazi mwenza atakayejihusisha na aina yoyote ya tabia ambayo inahusisha ukatili wa kijinsia, ikiwemo unyanyasaji wa kijinsia lakini badala yake huchangia kujenga mazingira salama kwa wote na kupaza sauti dhidi ya ukatili wa kijinsia, iwapo na pindi itakaposhuhudiwa.

Mameneja na wasimamizi watahakikisha kwamba wafanyakazi wote na wafanyakazi wenza wanafahamu na kufahamishwa kuhusu Sera na watahakikisha kuwa inaeleweka. Pia wana jukumu la kujumuisha jambo hili katika utambulisho wa wafanyikazi na wafanyikazi wenza wote wapya na kuhakikisha kwamba kila mtu anapatiwa mafunzo au kuhamasishwa kikamilifu na mara kwa mara kuhusu masuala ambayo Sera inayashughulikia. Wanawahimiza wafanyikazi kuripoti matukio na kushughulikia kila malalamiko haraka na kwa heshima na kwa usikivu. Mameneja na wasimamizi watafuatilia utekelezaji wa Sera hii inayopinga ukatili wa kijinsia na kuripoti kila mwaka kuhusu utiifu wa sera hii.

## Wajibu vikundi mahusus vya wadau

### Katibu Mkuu wa Ofisi ya Kimataifa ana wajibu wa

- kuzipatia Kamati zote za Kitaifa Sera ya ICYE ya "Usalama Pamoja",
- •kuhakikisha kwamba wawakilishi wote wa NC wamesaini Sera ya ICYE " Usalama Pamoja " ili kuonyesha kukubaliana kwao na maudhui yake,
- •kuhakikisha kwamba sera ya kimataifa inaboreshwa kadri inavyohitajika,
- •kutoa mafunzo ya mara kwa mara ya warsha za wakufunzi pamoja na mafunzo ya kujikumbusha,
- •kuwasaidia NC kuongeza ufahamu na kuwahamasisha wafanyakazi wote, kwa mfano kwa kutoa nyenzo za mafunzo,
- •hutayarisha ripoti ya utekelezaji wa Sera hii yenye taarifa zisizo na utambulisho kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia katika Shirikisho na jinsi zilivyoshughulikiwa kama sehemu ya ripoti ya mapitio ya mwaka

- kusaidia kutafuta fursa za fedha katika utekelezaji wa sera (kwa mfano zinazohitajika kwa ajili ya mafunzo, ushauri nasaha, msaada wa kisheria, wataalam),
- •kuendeleza kanzidata iliyoboreshwa ya wafanyikazi walioteuliwa katika kila NC iliyopewa jukumu la kushughulikia matukio ya ukatili wa kijinsia,
- •kuanzisha mfumo kwa ajili ya wafanyakazi wa kujitolea kutoa maoni kuhusu jinsi NC inavyotekeleza Sera ya ICYE ya " Usalama Pamoja ",
- •kuchukua hatua kulingana na Taratibu za Malalamiko za ICYE iwapo kuna migogoro.

## Bodi ya Mameneja ina wajibu wa

- kukuza sera ya ICYE ya " Usalama Pamoja " na utekelezaji wake,
- •kwa kushirikiana na IO kufuatilia utekelezaji wa Sera hii,
- •kuiboresha kila inapohitajika,
- •kuchunguza tathmini/mrejesho wa kila mwaka kutoka kwa wafanyakazi wa kujitolea,
- •kuchukua hatua kulingana na Taratibu za Malalamiko za ICYE iwapo kuna migogoro.

## Kamati ya Taifa ina wajibu wa

- kupitia, kusaini na kuwasilisha makubaliano yao ili kutekeleza Sera ya ICYE ya " Usalama Pamoja " kwenye Ofisi ya Kimataifa,
- •kuunda Kanuni za Maadili mahususi kwa nchi wanapoendesha shughuli zao na kuhakikisha kwamba wafanyakazi wote, wafanyakazi wenza na wafanyakazi wa kujitolea wanafuata kanuni hizi za maadili na ahadi za Sera hii,

- kumpa mtu mmoja ambaye anatumika kama mtu wa uwasiliana naye jukumu la kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia,
- kufanya uchunguzi unaostahili wakati wa kuajiri wafanyikazi, wafanyikazi wenza, wajumbe wa bodi zao, wafanyakazi wa kujitolea, familia mwenyeji na miradi mwenyeji ili kuhakikisha kwamba watu na mashirika yote yaliyochaguliwa yanakuwa na maadili sawa na ICYE,
- •kutengeneza mazingira salama ambapo wafanyakazi wa kujitolea wanajisikia vizuri kuzungumza na kushughulikia suala hilo,
- •kutekeleza utaratibu ulioandaliwa wa kuripoti na kukabiliana na masuala ya ukatili wa kijinsia, ikiwemo taratibu za wazi za kuwahamisha wafanyakazi wa kujitolea ambao wamehusika katika tukio la ukatili wa kijinsia iwe moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja
- •kuhifadhi kanzidata ya wataalam iliyoboreshwa (kwa mfano kuhusu ushauri nasaha, huduma za matibabu na sheria zenye uzoefu na zilizohamasishwa) katika nyanja hiyo ndani ya nchi yao kwa madhumuni ya marejeleo na kuwezesha msaada wa wowote wa kisheria au fidia ya kifedha ikihitajika kwa mujibu wa sheria pale tukio linapotokea
- •kupanga mafunzo kuhusu mada hiyo kwa ajili ya wafanyikazi, wafanyakazi wa kujitolea, familia mwenyeji na miradi mwenyeji. Warsha za mafunzo kwa wafanyakazi wa kujitolea zinapaswa kujumuisha mazungumzo ya uwazi na wafanyakazi wa kujitolea na NC wenzao kuhusu mambo ya hatari katika nchi zao na maeneo ya kujitolea. Mafunzo hayo yanapaswa kufanyika kabla ya hawajaondoka, mara tu baada ya kuwasili katika nchi mwenyeji na katika mpango mzima kama jukumu la pamoja la NC wanaotuma na wanaopokea,

- •kuongeza ufahamu kuhusu Sera ya ICYE ya " Usalama Pamoja " na mada hiyo pamoja na wafanyakazi wa kujitolea, miradi mwenyeji, familia mwenyeji na jamii mwenyeji.
- •kufuatilia masuala ya awali ili kuzuia upangaji ambao unaweza kuleta hatari kwa wafanyakazi wa kujitolea wa siku zijazo,
- •kufanya kazi ndani ya uwezo wao ili kujihami dhidi ya ulipizaji kisasi kwa mtu yeyote anayeripoti tukio,
- •kuripoti kwenye Ofisi ya Kimataifa angalau mara moja kwa mwaka kuhusu matukio ya ukatili wa kijinsia huku ukificha utambulisho wa watu waliohusika wakati wote
- •kutoa mbinu bora na kuwasaidia NC wengine katika ngazi za kikanda na shirikisho.

## Wafanyakazi wa ICYE wana wajibu wa

- kupitia, kusaini na kuwa na uelewe mzuri wa Sera ya ICYE ya " Usalama Pamoja ",
- •kutii Kanuni za Maadili zilizoundwa na NC yao mahususi,
- •uwe mfano wa kuigwa, kwa kuonyesha mfano kutokuwa mhalifu wala Mwezeshaji wa ukatili wa kijinsia, bali kuzungumzia kupinga unyanyasaji na ukatili wa kijinsia, ndani na nje ya kazi
- •kushiriki katika mafunzo kuhusu mada ya ukatili wa kijinsia
- •kuwa mwakilishi anayeaminiwa kwa wafanyakazi wenzake na wafanyakazi wengine
- •kufuata taratibu zote za kuripoti kwa uwazi, bila upendeleo, kwa uadilifu na kwa usiri,

- •kuwa msikivu, mwangalifu, mwenye busara, na mwelewa pale mtu anaripoti tukio,
- •kuwa tayari kutoa hati ya ukaguzi wa polisi au kumbukumbu binafsi ikihitajika,
- •wajulishe haraka wafanyakazi ndani ya shirika lao lililopewa jukumu la kushughulikia masuala yote ya ukatili wa kijinsia iwapo watapata taarifa kuhusu suala hilo.

## Wafanyakazi wenza wa ICYE wana waji wa

- kupitia, kusaini na kuwa na uelewe mzuri wa Sera ya ICYE ya " Usalama Pamoja ",
- •kutii Kanuni za Maadili zilizoundwa na NC yao mahususi,
- •usiwe mhalifu wala mwezeshaji wa ukatili wa kijinsia bali badala yake uwe mfano wa kuigwa, kwa kuonyesha mfano zungumzia ukatili na ukatili wa kijinsia, ndani na nje ya kazi
- •kushiriki katika mafunzo kuhusu mada ya ukatili wa kijinsia
- •kuwa tayari kutoa hati ya ukaguzi wa polisi au kumbukumbu binafsi ikihitajika
- •kuwa mwakilishi anayeaminika kwa wafanyakazi wa kujitolea
- •kuyatilia maanani matukio yote, kumsaidia mtu aliyeathirika, bila kujali ni jukumu alilonalo katika shirika

## Miradi mwenyeji wa ICYE una wajibu wa

- kupitia, kusaini na kuwa na uelewe mzuri wa Sera ya ICYE ya " Usalama Pamoja ",
- •kuhakikisha kwamba wafanyakazi wao na wafanyakazi wenza pia wanaifahamu sera na kuitekeleza sera hiyo. Iwapo miradi mwenyeji ina sera yake yenyewe ya kupinga ukatili wa kijinsia, hakikisha kwamba sera ya miradi mwenyeji na sera ya ICYE zinalingana,
- •kushiriki katika mafunzo ya ICYE kuhusu sera ya kuzuia na kukabiliana na ukatili wa kijinsia,
- •kujulishana wao wenyewe kuhusu tofauti za kitamaduni kuelekea tabia zisizofaa na kujidhatiti katika njia ya Uelewa wa Tamaduni Mbalimbali unapojihusisha na mada hii,
- kuelekea tabia zisizofaa na kujidhatiti katika njia ya Uelewa wa Tamaduni Mbalimbali unapojihusisha na mada hii,
- •kuzitilia maanani ripoti zote za masuala ya ukatili wa kijinsiana kuwasilisha masuala hayo kwa NC na wadau husika, baada ya idhini ya waathirika,
- •kutafuta na kushauriana na wataalam na mamlaka ili kuhakikisha kwamba hatua zote zinazofaa zinachukuliwa, bila kusababisha madhara au hatari zaidi, nje ya sera hii.

## Wafanyakazi wa Kujitolea wa ICYE wana wajibu wa

- kupitia, kusaini na kuwa na uelewe mzuri wa Sera ya ICYE ya " Usalama Pamoja ",
- •kuzingatia kanuni za maadili za NC mwenyeji,
- •kushiriki katika mafunzo kuhusu mada hii,

- •kuzingatia na kutii sheria na kanuni za nchi mwenyeji kuhusu suala hili,
- •kuzingatia na kutii sheria na kanuni za nchi mwenyeji kuhusu suala hili,
- •kujulishana wenyewe kuhusu sababu maalum za hatari za mahali husika na kuheshimu kanuni ambazo hazijatamkwa za nchi mwenyeji, kutohoa tabia zao ipasavyo,
- •kusikiliza mapendekezo ya familia/miradi/NC mwenyeji
- •kuwa mwangalifu na makini unapotumia mitandao ya kijamii kuelezea masuala ya ukatili wa kijinsia,
- •kuithibitishia NC kwa maandishi iwapo wataamua kutotafuta msaada kutoka NC ili kushughulikia suala la ukatili wa kijinsia.

## Familia Mwenyeji zina wajibu wa

- kupitia, kusaini na kuwa na uelewe mzuri wa Sera ya ICYE ya " Usalama Pamoja ",
- •kuzingatia kanuni za maadili za NC mwenyeji,
- •kushiriki katika vipindi vya mafunzo kuhusu mada hii,
- •kuelewa na kuelezea tofauti za tamaduni kuhusu urafiki, idhini na kukutana kimwili,
- •kuwajulisha wafanyakazi wa kujitolea kuhusu mambo ya hatari katika eneo lao,
- •kuwapa sehemu salama wafanyakazi wa kujitolea,
- •kuwasiliana na NC kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia ambayo mfanyakazi wa kujitolea anahusika na kujadili hatua za kuzichukua.

# Utekelezaji wa Sera hii

ICYE inafahamu kwamba ili kutekeleza sera hii kwa mafanikio ni muhimu

- kutafuta msaada kutoka kwa washauri wa nje
- kufahamu kwamba huu ni mchakato wa kudumu
- kuwajumuisha wafanyakazi na wafanyakazi wenza wote pamoja na washirika na wafanyakazi wa kujitolea katika mchakato wa kutekeleza sera hii.
- kuunda ufahamu na usikivu zaidi kwa ajili ya mada hii ndani ya NC na wafanyakazi wenza, familia na miradi mwenyeji.
- kuunda na kusambaza kitabu cha mawasiliano cha kimataifa ambacho mashirika ya mahali husika yanayoshughulikia suala hili yameorodheshwa.

## Msaada wa kifedha

Shirikisho na NC zimejitolea pia kutoa fedha zinazohitajika ili kutekeleza sera hii na watazijumuisha hizi katika bajeti zao.

Kupitia Mfuko wa TPD, Shirikisho litatoa nyenzo kwa ajili ya mafunzo ya kimataifa ya wakufunzi. Kamati Ndogo itaundwa ili kuandaa mwongozo wa mafunzo kwa msaada wa wataalam wa nje ili NC iutumie kuendesha warsha za mafunzo kwa wafanyakazi wao na wafanyakazi wenza.

# Ufuatiliaji na Tathmini

ICYE inatambua umuhimu wa kufuatilia utekelezaji wa sera hii. Itahakikisha kwamba inakusanya takwimu na data kuhusu jinsi inavyotumika na kama inafaa au la.

Zaidi ya hayo, ICYE itafuatilia utekelezaji wa sera hii kwa kuuliza maswali muhimu katika tathmini ya mtandaoni ya wafanyakazi wa kujitolea, Sehemu ya III.

Wasimamizi, mameneja na wale wanaohusika na masuala ya ukatili wa kijinsia katika Kamati za Taifa wataripoti bila utambulisho (bila kutaja jina la manusura) kwa kufuata sera hii, ikiwemo idadi ya matukio, jinsi yalivyoshughulikiwa, na mapendekezo yoyote yaliyotolewa kwa ICYE BoM na IO. Hili litafanyika kila wakati panapokuwa na suala la unyanyasaji wa kijinsia. Kulingana na ripoti hizi, shirika litatathmini ufanisi wa sera hii kwa msaada wa shirika la nje la wataalam na kufanya mabadiliko yoyote yanayohitajika.

# Fasili

**Idhini[9]:** inahusu "makubaliano kati ya washiriki kushiriki tendo la ndoa au kuingia kwenye ndoa. Ni lazima itolewe kwa uhuru na kikamilifu na haiwezi kutolewa na mtu ambaye amelewa madawa ya kulevya au pombe au na mtoto mdogo. Idhini ni mahususi, ikimaanisha kwamba idhini ya kitendo kimoja haimaanishi ni idhini ya kitendo kingine chochote, na inaweza kupinduliwa, ikimaanisha kwamba inaweza kubatilishwa wakati wowote.[9,10] Kiini cha idhini ni mawasiliano: Hapana inamaanisha Hapana na Ndiyo inamaanisha Ndiyo.

**Kinga ya Msingi:** inamaanisha mbinu ambazo hutumika kabla ya unyanyasaji wowote wa kijinsia kutokea ili kuzuia uhalifu na unyanyasaji awali. Kinga ya msingi ni pamoja na kujenga mazingira ambayo yanahimiza ustawi na njia nzuri."[11] Kinga ya msingi inaweza kukusudiwa kwa watu husika kwa jumla kwa mfano kushughulikia maadili ya kibaguzi au kuongeza ufahamu juu ya ukatili wa kijinsia , au inaweza kujumuisha mikakati ya kushirikiana na vikundi vilivyo katika mazingira magumu, kwa mfano watu waliobadili jinsia ambao wanakabiliwa na ukatili wa kijinsia au wanaoweza kuwa wahalifu ili kutafakari maadili ya hatari katika ukatili wa kijinsia.

9 Vidio bora ya elimu kuhusu idhini ni "Chai na Idhini" ("Tea and Consent"): https://www.youtube.com/watch?v=Exobo1GmYjs

10 https://www.unwomen.org/en/what-we-do/ending-violence-against-women/faqs/types-of-violence and https://www.rainn.org/articles/what-is-consent

11 https://www.atsa.com/sexual-violence-prevention-fact-sheet

**Ukatili wa kijinsia:** inafasiliwa kama "tendo lolote la ngono linalofanywa kinyume na mapenzi ya mtu mwingine, ama pale ambapo mtu huyu hajatoa idhini au pale ambapo idhini haiwezi kutolewa kwa sababu mtu huyo ni mtoto, ana ulemavu wa akili, au amelewa sana au amepoteza fahamu kwa sababu ya pombe au dawa za kulevya."[12] Ukatili wa kijinsia ni pamoja na kwa mfano ushawishi wa ngono usiohitajika au unyanyasaji wa kijinsia, ubakaji, utumwa wa ngono, udhalilishaji wa kijinsia.

**Unyanyasaji wa kijinsia:** "hujumuisha kushikwa mwilini bila ridhaa, kama vile kunyakuliwa, kubanwa, kupigwa makofi, au kusuguliwa na mtu mwingine kimahaba. Pia hujumuisha matendo mengine yasiyo ya mwilini, kama vile kuzomea, utani wa kijinsia kuhusu mwili au mwonekano wa mtu, kuhitaji upendeleo wa kimahaba, kukonyezwa kimahaba, kunyemelewa, na kuonyesha viungo vyake vya siri." [13] Pia inarejelea aina zote za udhalilishaji na ukatili wa kijinsia wa mtandaoni.

UN Women huangalia masuala yafuatayo inapozungumza kuhusu ukatili wa kijinsia:

- "unyanyasaji wa kijinsia ni suala la haki za binadamu, ni aina ya ubaguzi wa kijinsia, katika muktadha wa uhusiano usio sawa wa mamlaka;
- upo katika namna mbalimbali kuanzia shambulio la kingono hadi kuguswa kwa shari, udhalilishaji wa picha na matusi ya kijinsia na ubaguzi jinsia;

12 ibid, https://apps.who.int/iris/bitstream/handle/10665/77434/WHO_RHR_12.37_eng.pdf;jsessionid=99992B2729746A001D290C09AA2B2D53?sequence=1

13 https://www.unwomen.org/en/what-we-do/ending-violence-against-women/faqs/types-of-violence

- unyanyasaji wa kijinsia hufuata sura ya mamlaka na kukosekana usawa, makutano ya uke/ume/jinsia na tofauti nyingine za kimuundo za kijamii - rangi, kabila, umri, ulemavu, utaifa, dini na miundo mingine yoyote ya kijamii ambayo inawanyima fursa wanaonyanyaswa na kumpa upendeleo mnyanyasaji;;
- lugha inayotumika katika fasili haipaswi kupuuza, kutoa hukumu za kimaadili kupitia maneno kama vile maneno ya 'kuudhi', wala yasitumie vibaya madhara yanaweza kutokea;
- katika muktadha wa unyanyasaji wa kijinsia wa ajira unapaswa kueleweka kama kushiriki tendo la ndoa na/au ubaguzi jinsia usiokubalika;
- unyanyasaji wa kijinsia unajumuisha matukio mahususi, mienendo ya tabia na inaweza kuwa muktadha uliosambaa mahali pa kazi."[14]

ICYE inauchukulia unyanyasaji wa kijinsia kama kitendo cha ukatili. Tunapinga aina zote za kumlaumu mwathirika na hatutadharau wala kupuuza tabia hii.

Kwa kuwa ICYE inafanyakazi katika nchi kote ulimwenguni, tunaelewa kwamba kuna miktadha tofauti ya kitamaduni na kwamba baadhi ya tabia zinaweza kutambuliwa kwa njia tofauti. Kuzomea kwa mfano ni jambo la kawaida katika nchi nyingi na mara nyingi halichukuliwi kama unyanyasaji wa kijinsia na jamii. Ni muhimu kuan-

14 https://www.unwomen.org/-/media/headquarters/attachments/sections/library/publications/2020/discussion-paper-towards-international-standards-on-training-to-end-sexual-harassment-en.pdf?la=en&vs=2351

galia kwamba jambo hili ni aina ya unyanyasaji hivyo sio tabia inayokubalika. Wakati huo huo, tunatambua kwamba wafanyakazi wa kujitolea, familia mwenyeji au jamii kwa mfano wanaweza kuwa na mitazamo tofauti, hivyo ni wajibu wa ICYE kuongeza ufahamu miongoni mwa wafanyakazi wa kujitolea, familia wenyeji na jamii kuhusu jambo linalounda ukatili wa kijinsia.

**Wafanyakazi:** huchukuliwa kuwa wafanyakazi wote ambao wanalipwa.

**Wafanyakazi wenza:** ni watu wanaofanya kazi na Kamati ya Kitaifa kwa hiari, kama vile wafanyakazi wa kujitolea, washauri, washirika.

**Familia za Mwenyeji za ICYE:** ni watu ambao huwapa makazi Wafanyakazi wa Kujitolea wa ICYE katika kipindi chao cha huduma ya kujitolea kimataifa.

**Miradi ya Mwenyeji ya ICYE:** ni mashirika ya mahali husika ambayo huwakaribisha wafanyakazi wa kujitolea wa ICYE katika nchi hiyo.

**ICYE: Wafanyakazi wa Kujitolea:** ni wafanyakazi wote wanaojitolea wa Kimataifa waliochaguliwa kushi¬riki katika mpango wa ICYE Exchange.

**Ofisi ya Kimataifa ya ICYE**
Große Hamburger Straße 30
D-10115 Berlin
Ujerumani

Simu: +49-30-28 39 05 51

www.icye.org

icye@icye.org

www.facebook.com/icyeio

www.instagram.com/icye.federation